OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MKINGA.

SHULE YA SEKONDARI DALUNI
S.L.P 91,
MARAMBA - TANGA
TAR_____

KUMB: Na HW/MKG/S.2743/...../..../ VOL.1.....

MWANAFUNZI .....
S.L.P .....
.....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI DALUNI WILAYA YA MKINGA MWAKA 2021.

1.0: Nafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule ya Sekondari Daluni mwaka 2021. Shule hii ipo Kata ya Daluni Kijiji cha kisiwani B katika Kitongoji cha Kiwanjani.
Muhula wa masomo utaanza tarehe..... Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11/01/2021 .

2.0: **MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

2.1 **Sare ya shule**

2.1.1 **Wavulana**

a) Suruali mbili (2) damu ya mzee kitambaa aina ya istem mashono ya kawaida(model/ya kubana hazitakiwi)
shati nyeupe mbili (2) mikono mifupi viatu vya ngozi jozi mbili (2) vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi, soksi nyeusi ndefu jozi mbili na mkanda mweusi wa kawaida.

2.1.2 Wasichana

Sketi mbili (2) damu ya mzee marinda kuanzia tumboni ziwe na mikanda usiyozidi sentimita nne , shati mbili nyeupe za mikono mifupi, viatu vya ngozi jozi mbili (2) vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi, soksi nyeupe jozi mbizi . Kwa wasichana wanaopenda kuvaa Hijabu lazima ifanane na sare ya shule yetu.

2.1.3 Sare za michezo

- Wavulana waje na flana nyekundu, bukta nyeusi, traksuti nyeusi na raba
- Wasichana waje na flana nyekundu , traksuti nyeusi na raba

2.2 VIFAA

- Begi mathubuti la kubebea daftari na vifaa vingine vya taaluma
- Daftari kubwa zisizopungua kumi na moja (11)
- Mkebe kwa ajili ya vifaa vya hisabati na jiografia
- Rula
- Kalamu za wino 2 na penseli 2

2.3 VIFAA VYA USAFI

- Fagio la njiti (chelea)
- Aje na .....
- Ndoo 1
- Picha 4 aina ya paspoti.

3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na 25 ya mwaka 1978, aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na TAMISEMI na Wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo:-

i. Heshima kwa viongozi, walimu ,wazazi, wafanyakazi wasio walimu na wanafunzi wengine na jamii kwa jumla.
ii. Kuhudhuria shuleni kwa mujibu wa sheria na taratibu za shule.
iii. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa, pamoja na kutii kengele.
iv. Kufahamu mipika ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hi.i
v. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
vi. Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa kufanya hivyo.
vii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
viii. Hairuhusiwi mwanafunzi;
- Kuwa na kucha ndefu.
- Kujipamba mwili.
- Kufuga ndevu.
- Kunyoa au kuchonga nyusi.
- Kufuga nywele ndefu na kunyoa kipara

3.1. Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha mwanafunzi kufukuzwa shule:-

1) Wizi
2) Uasherati
3) Ubakaji
4) Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli,heroin nk
5) Kupigana au kupiga
6) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
7) Kudharau bendera ya Taifa
8) Kuolewa au kuoa
9) Kutoa mimba
10) Kupata mimba, kusababisha mimba ndani au nje ya shule
11) Kugoma, kuchochea au kuongoza migomo na kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
12) Kukataa adhabu, kugomea adhabu
13) Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi

3.2 Hitimisho

Tafadhali soma kwa makini maelekezo na maagizo yote hapo juu na kuyatekeleza kikamilifu .

Aidha, kama unakubali kujiunga na shule hii baada ya kusoma maelezo na maagizo haya, jaza fomu ambazo zimeambatanishwa na maelekezo haya wewe binafsi pamoja na mzazi/mlezi wako na vilete utakapokuja kuripoti hapa shuleni

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI DALUNI

.....

MALOWI AGRIPINUS J.
MKUU WA SHULE

PRESIDENT'S OFFICE

REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL AUTHORITIES

MKINGA DISTRICT COUNCIL

DALUNI SECONDARY SCHOOL

To be completed by the medical officer in respect of FORM I entrants:

Pupil's full name .....

Age.....

Blood Group (red and white).....

Stool Examination.....

Urine Analysis.....

Syphilis Test.....

T.B Test .....

Ears.....

Chest.....

Spleen.....

Abdomen.....

AUDDITIONAL INFORMATION: e.g. Physical defects or impairments

Infections chronic of family disease etc.

.....

.....

.....

.....

.....

I certify that the above concern is fit /unfit for admission into a Day/Boarding school;

Signature.....

Designation.....

Station .....

Date .....

OFFICIAL STAMP

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

FOMU YA KUKUBALI NAFASI ULIYOOMBA - AHADI YA MWANAFUNZI

.....
.....
.....
.....

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI DALUNI
S.LP 91, MARAMBA
TANGA.

Barua yenu ya tarehe..... nimeipata na ningependa kuwahakikishieni kuwa nimekubali/siikubali nafasi hiyo niliyopewa kuingia kidato cha kwanza mwaka .....

a) Nitaleta vifaa vya muhimu vilivyotajwa katika barua
b) Nitazitii na kuzingatia sheria za shule kama itakavyoamriwa na walimu na wote wanaohusika kwa kufuatana na matakwa ya shule za serikali yetu.

Jina la mwanafunzi (mwanao).....
Jina la mzazi/mlezi.....